**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**06** **URAIA NA MAADILI**

**Muda: Saa 1:30** **SULUHISHO** **Mwaka: 2019**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu mbili; A na B zenye jumla ya maswali **sita (06)**
2. Jibu maswali **yote**


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org

*Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA*

**SEHEMU A (Alama 26)**

1. Jibu vipengele (i) – (v)

(i) Unapaswa kufanya nini unapoishi na watu wenye tabia zisizokubalika katika jamii?
A. Kuwakimbia bila kuwashauri
B. Kuwavumilia na kuwashauri
C. Kupigana nao hadi wabadilike
D. Kuwatolea maneno makali
**Jibu: B. Kuwavumilia na kuwashauri**
Sababu: Kuwashauri na kuwatendea kwa uvumilivu kunasaidia kubadilisha tabia zisizokubalika bila kuleta migongano.

(ii) Njia ipi inaweza kutumika katika kutatua changamoto zinazokukabili?
A. Kuzikubali na kuweka malengo
B. Kuwa ombaomba na kutaka ushauri
C. Kuchoka na kukata tamaa
D. Kuweka malengo na kuyaacha
**Jibu: A. Kuzikubali na kuweka malengo**
Sababu: Kukubali changamoto na kupanga malengo kunasaidia kupata suluhisho kwa tatizo.

(iii) Lipi kati ya matendo yafuatayo yanaonesha tabia ya ustahimilivu?
A. Kudadisi bila kuchoka na kupata jibu
B. Kufanya kazi kwa bidii na kupumzika sana
C. Kufanya kazi haraka haraka
D. Kufanya kazi polepole
**Jibu: A. Kudadisi bila kuchoka na kupata jibu**
Sababu: Ustahimilivu ni kudumisha juhudi bila kuchoka hata changamoto zipo.

(iv) Kuhimili vikwazo katika maisha kunatuwezesha kufikia
A. matatizo yetu ya kila siku
B. heshima yetu
C. ugumu wa maisha
D. malengo yetu
**Jibu: D. malengo yetu**
Sababu: Kuhimili vikwazo kunasaidia kufanikisha malengo ya maisha.


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org
***Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA***

(v) Hali ya kujiamini na kutarajia mafanikio katika jambo fulani hujulikana kama
A. Udadisi
B. Changamoto
C. Mtazamo chanya
D. Uvumilivu
**Jibu: C. Mtazamo chanya**
Sababu: Mtazamo chanya unaonyesha kujiamini na matarajio ya mafanikio.

2. Jibu vipengele (i) - (iv) kwa kuoanisha alama za Taifa.

(i) Huonesha utajiri wa mali asili ya nchi yetu.
**Jibu: F. Pembe za ndovu**

(ii) Hutumika katika barua za kiofisi na machapisho ya serikali.
**Jibu: E. Fedha za Tanzania**

(iii) Huashiria uhuru wa nchi yetu.
**Jibu: C. Wimbo wa taifa**

(iv) Huwakilisha vifaa vinavyotumika kuendeleza taifa.
**Jibu: B. Jembe na nyundo**

3. Chagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano.

(i) Kitendo cha mtoto kushiriki katika maamuzi huonyesha
**Jibu: wajibu wa mtoto**

(ii) Ili watoto wapate msaada mara wanapohitaji wanatakiwa wawe:
**Jibu: wakweli**

(iii) Lipi kati ya yafuatayo ni wajibu wa mtoto?
**Jibu: kufanya kazi rahisi**

(iv) Kitendo cha mtu kufanya kazi aliyopangiwa huitwa
**Jibu: uaminifu**

## SEHEMU B (Alama 24)

4. Jibu vipengele (i) – (v) kwa kuweka alama ya vema (√) kuonesha kama zana ni za asili au siyo za asili.

(i) Gitaa – Zana zisizo za asili √


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org
***Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA***

(ii) Manyanga – Zana za asili √

(iii) Kinanda – Zana zisizo za asili √

(iv) Filimbi – Zana zisizo za asili √

(v) Tarumbeta – Zana zisizo za asili √

5. Chunguza picha na jibu maswali.

(i) Ni kitendo gani kinaoneshwa katika picha?
**Jibu:** Kutumia au kuimba muziki

(ii) Unafikiri kwanini mtu huyu katika picha anafanya kitendo hiki?
**Jibu:** Ili burudisha au kufundisha wengine muziki

(iii) Ni hasara gani inayosababishwa na kitendo kinachofanyika katika picha?
**Jibu:** Kama zana hazitunzwa vizuri zinaweza kuharibika

(iv) Pendekeza njia mojawapo ya kulinda na kutunza mazingira ya eneo liliooneshwa kwenye picha
**Jibu:** Kuweka zana na vifaa kwenye sehemu salama na safi, kuzuia uchakavu

6. Soma kifungu cha habari kisha jibu maswali.

Vyanzo vya maji ni muhimu katika maisha yetu. Mfano wa vyanzo vya maji ni mito, maziwa, bahari, mabwawa, visima, mvua na chemichemi. Tunapaswa kuvilinda vyanzo hivi vya maji. Tunaweza kuvilinda vyanzo vya maji kwa kutokata miti ovyo kandokando ya vyanzo vya maji, kupanda miti, kutojisaidia au kutupa taka kwenye vyanzo vya maji. Maji yanatumika kwa kunywa, kupikia, kuoshea, kuoga, kusafisha na kumwagilia mazao. Ni wajibu wa jamii nzima kuvilinda vyanzo vya maji.

(i) Kulingana na kifungu hiki cha habari, mito, maziwa, bahari, mabwawa na mvua huitwa
**Jibu:** Vyanzo vya maji

(ii) Ni nani anawajibika kulinda vyanzo vya maji?
**Jibu:** Jamii nzima

(iii) Tunawezaje kuvitunza vyanzo vya maji?
**Jibu:** Kutokata miti ovyo kandokando ya vyanzo vya maji, kupanda miti, kutokutupa taka kwenye vyanzo vya maji

(iv) Tunatumia maji kwa shughuli zipi?
**Jibu:** Kunywa, kupika, kuoshea, kuoga, kusafisha na kumwagilia mazao


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org
***Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA***